

Taarifa ya COVID-19 ya Jiji la Burlingtons

Kituo cha Rasilimali na Kupona kwa COVID-19 cha Burlington (RRC)

Januari 2021

Kiswahili

Aina Mpya za COVID-19



Mabadiliko mapya ya virusi vya korona yametokea. Huku iligunduliwa ya kwanza Uingereza, sasa inapatikana katika nchi nyingi ikijumuisha yetu pia. Maafisa wanatarajia kuwa aina hiyo itatambuliwa katika Vermont hivi karibuni. Mabadiliko ya virusi ni ya kawaida, kama vile na mabadiliko ya mafua kutoka mwaka hadi mwaka, lakini kinachofanya haya kuwa tofauti ni kuwa yanaenea kwa haraka zaidi kuliko aina asilia ya COVID-19. Kutakuwa na mambo mengi yasiyojulikana kuhusu hatari ya aina hii mpya ya COVID-19 kwa wakati huu. Hii inamaanisha kuwa wanachama wa jumuiya yetu wanaweza kuwa katika hatari iliyoongezeka ya kuambukizwa virusi, watu zaidi huenda wakajipata hospitalini, na tunaweza kuona ongezeko la vifo katika Vermont. Paa taarifa na visasisho zaidi kuhusu aina mpya ya COVID-19 kwenye wavuti wa CDC.

Usambazaji wa Chanjo

Kama baadhi yenu huenda wamesikia, sasa kuna chanjo mbili za COVID-19 ambazo zimeidhinishwa kwa matumizi katika Marekani, Moderna na Pfizer. Hapa ni baadhi ya vitu vichache vya kujua:

- Vermont ipo katika awamu za mapema za usambazaji wa kutoa chanjo kwa wahudumu wa afya wa mstari wa mbele na watu walio katika mipangilio ya huduma ya afya ya mtagusano wa karibu. Kikundi kinachofuata kitakuwa cha watu wazee zaidi katika jumuiya yetu na watu walio katika hatari zilizoongezeka za ugonjwa mkali.
- Zaidi ya watu 20,000 katika Vermont wamepokea dozi ya chanjo ya kwanza kufikia Januari 8, na wataendelea kuongezeka jinsi Jimbo litakavyoendelea kupokea dozi zaidi za chanjo hiyo.

- Chanjo za sasa zilizoidhinishwa zinapeanwa kwa dozi mbili tofauti, kwa umbali wa wiki tatu hadi nne.
- Bado hatujui ni lini chanjo hiyo itapatikana kwa upana. Makadirio ya kitaifa kwa msambao wa upatikanaji wa chanjo kwa umma wa kawaida ni kuanzia Aprili hadi katikati ya msimu wa joto 2021. Kwa watoto walio na umri wa chini ya miaka 16, upatikanaji wa chanjo unaweza kuchukua muda hata zaidi kwa sababu utafiti bado unaendelea kwa watu wa umri wa chini.
- Chanjo hizi maalum ni chanjo za mRNA (Messenger RNA), ambazo hufunza na kutuma maelekezo kwa seli zetu kuhusu jinsi ya kupigana na maambukizo. mRNA kamwe huwa haiingii katika kiini (kitovu) cha seli, ambayo ni sehemu ambayo nyenzo ya jeni huhifadhiwa, haitaathiri au kubadilisha DNA yako. Chanjo hii pia si virusi vilivyo hai na kwa hivyo haiwezi kukuambukiza COVID-19.

Ukiwa na maswali kuhusu chanjo hiyo, mhudumu wa afya anayefanya kazi na familia yako anaweza kusaidia kuyajibu. Ikiwa huwezi kufikia mhudumu wa afya, unaweza kuwasiliana na Kituo cha Rasilimali na Kupona cha Jiji na tutafanya tuwezalo ili kukuunganisha na taarifa unayohitaji kutoka kwa chanzo cha matibabu ya kitaalamu.

Kitu bora zaidi ambacho sote tunaweza kufanya ni kukaa macho na kulinda familia na majirani kwa kuendelea kuvaa barakoa zenye safu anuwai, kunawa mikono yako mara kwa mara, kukaa mbali na wengine, na kuepuka mikusanyiko ya kijamii. Ikiwa ulihudhuria mikusanyiko yoyote ya kijamii, Idara ya Afya ya Vermont inapendekeza kwenda kupimwa mara moja baadaye sawa na siku 7 baada ya tukio hilo. Ikiwa unahitaji barakoa, tafadhali wasiliana na RRC. Sote tupo pamoja kwa hii.

Msaada wa Kupitisha Hewa



Vifaa vya kusafisha hewa vimeonyeshwa kuwa vinaondoa baadhi ya chembe za virusi kwenye hewa na kusaidia kupunguza – lakini si kuondoa! – hatari ya usambazaji katika mipangilio ya ndani ya nyumba. Jiji la Burlington litazindua mpango mpya wa msaada wa kupitisha hewa katika juhudi ya kutoa vitengo vya kuchuja hewa bila malipo kwa nafasi za Burlington za biashara na mashirika yasiyo ya kifaida ambapo

jamii kadhaa zinaweza kutagusana. Wapokeaji wa msaada huo watapokea usaidizi katika kununua na kusakinisha kifaa cha kuchuja hewa. Programu hiyo itafunguliwa kwa wiki moja, kuanzia Jumatatu Januari 11 hadi Januari 18, 2021. Maombi ya kuchelewa yatakubaliwa, lakini usambazaji unaweza kuwa umeisha. Kwa maswali au usaidizi wa tafsiri, tafadhali wasiliana na BTVEmployer@burlingtonvt.gov. Ikiwa unapendelea usaidizi wa lugha kwa simu, unaweza kupigia RRC kupitia 802-755-7239.

Wavuti wa Msaada: https://www.burlingtonvt.gov/covid-19/ventilation-grant (Kiingereza)

Kipimo

Upatikanaji wa kipimo umeongezeka na kinapatikana kila siku katika Burlington (405 Pine St.) na Winooski (32 Mallets Bay Ave), na vituo vya ziada katika mwezi mzima. Ikiwa una matatizo ya kujisajili, unaweza kupigia meneja wa kisa chako simu katika AALV au USCRI, au wasiliana na RRC, na tutajitahidi ili kukusaidia bora. Inayofuata ni orodha ya chaguo za kipimo:

Kila Siku - Studio ya Sanaa katika Jiji la Burlington - 405 Pine St, Burlington VT, 05401

Kituo cha kipimo kipo katika nafasi iliyo karibu na studio ya Sanaa katika Jiji la Burlington katika 405 Pine Street
Kinafanya kazi kila siku: 12:00pm-8:00pm kila siku
Huduma za mkalimani ndani ya kituo zinapatikana wakati wowote kila siku
Usajili wa mapema unapendelewa

Kila siku - Kituo cha Jumuiya cha O'Brien - 32 Malletts Bay Ave, Winooski VT, 05404

Huduma za mkalimani ndani ya kituo zinapatikana
Kipimo hufanya kazi kila siku, Jumatatu - 5:00pm-8:00pm, Jumanne-Jumapili 9:00am-3:00pm
Usajili wa mapema unapendelewa

Burlington North End Studios – 294 North Winooski Ave, Burlington VT, 05401

Vituo vya kughafla vitafanya kazi 9:00am-3:00pm
Huduma za mkalimani ndani ya kituo zinapatikana
Januari tarehe 15 – jisajili mapema au uhudhurie tu
Januari tarehe 22 – jisajili mapema au uhudhurie tu
Januari tarehe 29 – jisajili mapema au uhudhurie tu

Colchester Malletts Bay Congregational Church - 1672 W Lakeshore Dr, Colchester, VT 05446

Vituo vya kughafla vitafanya kazi 9:00am-3:00pm
Huduma za mkalimani kupitia kwa simu zinapatikana
Januari tarehe 14 – jisajili mapema au uhudhurie tu
Januari tarehe 21 – jisajili mapema au uhudhurie tu
Januari tarehe 28 – jisajili mapema au uhudhurie tu

Williston National Guard Armory - 7846 Williston Rd, Williston VT, 05495

Vituo vya kughafla vitafanya kazi 9:00am-3:00pm
Huduma za mkalimani kupitia kwa simu zinapatikana
Januari tarehe 13 – jisajili mapema au uhudhurie tu
Januari tarehe 27 – jisajili mapema au uhudhurie tu

Maswali? Je, Unahitaji Usaidizi?

Kituo cha Rasilimali na Kupona kwa COVID-19 cha Burlington kiko hapa kukusaidia, wasiliana nasi kupitia 802-755-7239 au recovery@burlingtonvt.gov na uache ujumbe wenye jina lako, lugha unayopendelea, na maelezo ya mawasiliano na tutakusaidia haraka iwezekanavyo. Kituo chetu cha kupokea simu kina huduma za ukalimani kwa simu. Saa zetu za kufanya kazi ni Jumatatu hadi Ijumaa, 8:00am-4:30pm.

Sifa kwa:
CDC
https://www.cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/transmission/variant.html
https://www.cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/vaccines/index.html
Idara ya Afya ya Vermont
https://www.healthvermont.gov/media/translation/covid-19-translations (pata taarifa iliyotafsiriwa kuhusu COVID-19)
https://www.healthvermont.gov/covid-19/testing/where-get-tested
https://www.healthvermont.gov/covid-19/vaccine
Jiji la Burlington
https://www.burlingtonvt.gov/covid-19/ventilation-grant
https://www.burlingtonvt.gov/covid-19/testing
https://www.burlingtonvt.gov/resources

Picha kutoka CDC na Jiji la Burlington